

MAPAMBAZUKO YA PASAKA

 ...katika machozi, huja kwa furaha. Amina. Loo, kwa sababu Mimi ni hai ninyi pia mtaishi. Loo jamani, kama watakatifu wa Agano la Kale wangeweza kuwazia hilo, inatupasa sisi kuwazia nini asubuhi ya leo, baada ya miaka elfu moja mia tisa ya kuona mateso na taabu na kadhalika; tukijua ya kwamba tuko moja kwa moja kwenye mlango wa mbele wa ufufuo. Amina. Kanisa limesonga mbele moja kwa moja kufikia kwenye majira sasa ambapo ufufuo unaweza kuja wakati wowote. Nami ninawazia itamaanisha nini kwetu siku hiyo, waaminio, itamaanisha nini kwako siku hiyo.

² Ninaweza kuona ile asubuhi na mapema wakati Martha na Mariamu walipotoka kwenda kaburini. Walikuwa wakija kando ya kilima baada ya usiku... Wazia juu ya moyo wa maskini mama huyo. Mtoto wake kote kote, wakati alipokuwa... wakati alipozaliwa, walisema alikuwa ni Mtoto haramu, ya kwamba kabisa hakuwa wa Yusufu, na—na alikuwa, ama, alikuwa ni wa Yusufu, nao walikuwa...huyo Mtoto mchanga alizaliwa nje ya ndoa takatifu. Alikuwa na hayo yote ya kupitia, na ninii, yote, “lile jambo kuhusu mtoto wako mchanga,” na jinsi alivyokuwa amekataliwa, na kudharauliwa, na kutemewa mate, hata hivyo Yeye alilidai. Naye, kwa namna fulani, kwa moyo wake unaotetemeka, akasema, “Mungu aliniletea Mtoto huyo mchanga, ingewezekanaje?” Akimwona Yeye kule katika saa hiyo muhimu sana.

³ Aliwazia bila shaka, walipoenda kumvika taji ya miiba kichwani Mwake, na kumpiga mpaka Damu ikatokea mgongoni Mwake, wakamvua nguo kabisa na mambo haya yote; aliwazia hakika ya kwamba wakati wowote Yeye atauangusha msalaba huo chini na kugeuka, akanyage chini ardhini kwa mguu Wake (dunia itatetemeka kutoka upande mmoja hadi mwingine) na kutangaza kwamba Yeye alikuwa ni Nani. Lakini Yeye alikuwa amefia huko, kama maskini mhalifu aliyeshindwa, akitundikwa msalabani.

⁴ Alikuwa amekufa katika aibu. Ninyi bila shaka huiona ile picha akiwa amefungwa kitambaa, hiyo ilikuwa ni makosa. Walimvua kila kipande cha nguo, kwa ajili ya ninii tu...na kumfedhehi kwa walimwengu na kila kitu walichoweza, kisha wakampiga misumari msalabani.

Na hapo alionekana amesimama bila usaidizi. Akisimama, dunia haikumtaka, Mbingu isingeweza kuwa Naye, Yeye alikuwa ni mwenye dhambi. Loo jamani! Laiti ungalitambua, wazia tu, dunia haikumtaka Muumba wake. Mbingu hazingeweza kumpokea kwa sababu alikuwa ameibeba dhambi ya dunia.

Hata hawakuwa na mahali . . . nena kuhusu mahali pa kuzaliwa, Yeye hakuwa na mahali pa kufia. Hiyo ni kweli. Dunia haikumtaka. Walikataa, kasema, “Mwondoeni jamaa kama huyo.” Mbingu hazingeweza kumpokea kwa sababu tayari alikuwa, alikuwa ni mwenye dhambi.

⁵ Loo, ni Mwokozi wa—wa jinsi gani! Akitoka Utukufuni na kuwa hivyo kwangu. Alikataliwa kabisa na walio Wake, hata, “Alikuwa kwa walio Wake, walio Wake hawakumpokea.” Yeye, hakuna mahali pa kuzaliwa, hakuna mahali pa kufia. Ulimwengu ulitaka nini Kwake? Wangeweza kufanya nini ila kumtupa Yeye kuzimuni.

Lakini kulikuwa na Mtu aliyempenda. “Sitaiacha nafsi Yake katika kuzimu, wala sitamwacha aone uharibifu.” Lakini Yeye alimfufua kutoka kaburini, Naye akafufuka kwenye asubuhi ya Pasaka, akiwa mshindi. Haleluya! Akavunja kila kizuizi na kila hofu na kitu, akafufuka tena na amesimama akiwa hai leo, milele.

⁶ Uwepo Wake upo hapa, Yeye yuko mahali hapa asubuhi hii ya ibada. Yeye hukutana popote wawili watatu wamekusanyika pamoja. Unajua jinsi nilivyo na moyo wenye furaha, kujua ya kwamba ahadi zile alizofanya katika Biblia, “Mambo nifanyayo Mimi, ninyi nanyi mtayafanya. Nitakuwa pamoja nanyi hata mwisho wa ulimwengu.” Watu maskini, waliokataliwa, waliodharauliwa na ulimwengu huu bado tunaweza kuwa na Uwepo Wake pamoja nasi. Mweza yote, aliye kila mahali daima, aliyepo daima, mwenye nguvu zote, kila mahali wakati wote. Jinsi alivyofanya njia ya kuepukia, katika kila saa ya shida. “Mimi ni Msaada upatikanao wakati wa shida,” Yeye alisema.

⁷ Sasa, asubuhi ya leo Yeye yu hai. Yuko pamoja nasi leo. Huenda tukawa kanisa dogo tu leo, huenda tukawa ni maskini maskini ndogo iliyojaa watu, haina uzuri wa kutazamwa; lakini kamwe hakuna mahali panyenyekevu kupita kiasi, ila ambapo atapajia. Yu hai leo miongoni mwa walio hai. Yeye hajafa, bali yu hai. Naye anaishi miongoni mwa walio hai.

⁸ Rafiki mwenye dhambi, leo, kama umekufa katika dhambi na makosa, kwa nini usiishi? Kwa nini unakaa katika mauti? Nini . . . umepata faida gani kwa kukaa mautini? Kwa nini usije kwenye uhai? Kwa nini usiishi pamoja Naye leo? na kwa tumaini hili kuu lililobarikiwa, ambapo hata mauti yenyewe, yakijitenga na wapendwa wenu, hayawezi kamwe kutia doa ama kuharibu au kuondoa chochote kutoka kwenu?

Ni tumaini lenye baraka jinsi gani. Ni kitu cha ajabu jinsi gani tulicho nacho leo hii, kwa sababu ya kufufuka Kwake. Naye yu hai, nasi tunaishi pamoja Naye, na siku moja atakuja, nasi tutaenda Naye. Kwa kuwa, alisema, “Enendeni mkawaambie

wanafunzi Wangu na Petro ya kwamba nitawatangulia kwenda Galilaya.”

⁹ Yeye daima huenda mbele yetu kutengeneza njia. Mahali pasipo na njia, Yeye alisema, “Mimi ndimi Njia. Mimi ndimi Ufufuo, Mimi ndimi Uzima.” Na jalia, leo, tunapokusanyika hapa leo... Mnampenda?

Yu hai, Yu hai, Kristo Yesu yu hai leo!
Hutembea pamoja nami, huzungumza nami,
katika njia nyembamba ya maisha.
Yu hai, Yu hai, kutupa wokovu!
Unaniuliza ninajuaje Yeye yu hai? Anaishi
ndani ya moyo wangu.

¹⁰ Je, hilo si ni la ajabu? Ni wangapi walio na tumaini hili lililobarikiwa asubuhi ya leo, utainua mkono wako? Hakika. Kuna mmoja hapa asiye na tumaini, ambaye angesema, “Ndugu Mhubiri, asubuhi ya leo, wewe katika kusanyiko hili, nikijua ya kwamba nimekusanyika pamoja nanyi hapa kwenye asubuhi ya ufufuo, na hata hivyo, hakuna Uhai usiopatikana na mauti unaokaa ndani yangu, wala tumaini hili haliko kifuani mwangu. Ningependa ninyi nyote mnikumbuke leo katika maombi kwamba huu utakuwa ndio ufufuo ndani yangu, kwamba nafsi yangu itafufuliwa katika tumaini hili la ajabu nikijua ya kwamba siku moja sina budi kubinya mto wa kufa na sina budi kuzikwa makaburini mahali fulani, makaburini, ama huko nje baharini, ama popote itakapokuwa kura yangu kuangukia; bali ninataka kuwa na tumaini hilo. Ninainua mkono wangu na kuwaomba mniombe?” Kuna mtu? Waweza kuinua mkono wako wewe usiye na...? Nadhani ninyi nyote ni Wakristo basi. Hilo ni zuri sana. Hebu... .

¹¹ Ninaamini leo, baada ya kurudi, kurudi, ninaamini ya kwamba Mungu Mwenyezi atamtuma Bwana Yesu hapa kwenye jukwaa hili leo, na atawathibitishia bila shaka ya kwamba Yesu yu hai na miongoni mwa watu leo. Amina. Ninajua Yeye yuko papa hapa sasa. Amina. Yuko hapa. Yu hai. Tunamwona. Sisi... . Yeye alimwambia Tomaso, “Ni kubwa vipi thawabu yao wale ambao hawajawahi kuniona Mimi na hata hivyo wanaweza kuamini.” Amina. Yeye ni wa ajabu.

¹² Sasa, hebu tuimbe huu. Tupe sauti, Dada Gertie, juu ya huo, *Yeye yu Hai*. Ninapenda tu kusikia huo ukiimbwa asubuhi ya leo. Loo, tunaona huzuni na taabu na jinsi gharama ilivyokuwa, lakini sasa, wazia tu, yote yamekwisha. Haleluya. Mchana umefika. Kuzimu imekwisha. Kaburi halipo tena. Mauti ni kwa ajili ya enzi. Giza lote limetoweka. Tunaishi. Amina. Tunaishi Naye anaishi. Yeye yu hai, nasi tunaishi ndani Yake. Amina. Sote pamoja sasa:

Yu hai, Yu hai, Kristo Yesu yu hai leo!

Naye hutembea pamoja nami na kuzungumza
 nami katika njia nyembamba ya maisha.
 Yu hai, Yu hai, kutupa wokovu!
 Unauliza . . . ninajuaje . . . ?

Njoo sasa.

. . . anaishi ndani ya moyo wangu.

Kila mtu, kwa sauti kubwa uwezavyo sasa:

Yu hai, Yu hai, Kristo Yesu yu hai leo!
 Naye hutembea pamoja nami, huzungumza
 nami katika njia nyembamba ya maisha.
 Yu hai, Yu hai, kutupa wokovu!
 Unaniuliza ninajuaje Yeye . . . ?

Inua mkono wako sasa.

. . . anaishi ndani ya moyo wangu.

¹³ Peana mikono na mtu aliyekei karibu nawe na useme, “Bwana asifiwe.” Ninyi nyote ni Wakristo. Wewe ni raia mwenzangu. Loo, jamani. Hilo haliwafanyi kujisikia vizuri? Ya nyuma yote yamesahauliwa, yote yamekwisha. Ni nani aliyefanya jambo hilo? Yeye yu hai, alifanya hivyo. Nani alifanya hivyo? Kristo. Hebu tuuimbe tena, sasa, kwa sauti yetu yote.

Yu hai, Yu hai, Kristo Yesu yu hai leo! (Hofu zote zimetoweka!)
 . . . pamoja nami na Yeye huzungumza nami
 katika njia nyembamba ya maisha.
 Yu hai, Yu hai, kutupa wokovu!
 Unaniuliza ninajuaje . . . ? (Angazeni sasa.)
 Anaishi ndani ya moyo wangu.

¹⁴ Loo, jamani. Huo si ni mzuri sana? Kwa namna fulani, nyingine, huo una mlio maalum kwangu asubuhi ya leo. Sauti zenu zote zikiungana pamoja, zinasikika za kupendeza sana. Mliona hilo? Inaonekana tu kana kwamba kweli inatoka kwenye kilindi cha moyo wako.

¹⁵ Masumbuko ya wakati uliopita yamekwisha sasa. Ufufuo umethibitishwa. Yesu amefufuka katika wafu, na Yu hai, nami ninaishi pamoja Naye. Amina. Anatutokea, na kuzungumza nasi njiani; anatuonyesha maono, mambo yaliyopita, na mambo yatakayokuja. Yeye huponya magonjwa yetu na kutupa furaha. Anatupa amani. Na wakati mauti yanapokodoa macho usoni, tunapaza sauti, “Sitaogopa mabaya, kwa kuwa Wewe u pamoja nami.” Jinsi ninavyopenda hilo! “Loo, mauti, u wapi mwiba wako? Kaburi, u wapi ushindi wako? Ninatoka kwenye ushindi hadi ushindi.” Je, kifo ni ushindi? Kabisa, mauti ni ushindi. Amina. Mauti ni ushindi sasa, si huzuni. Ni, vema, ni ushindi. Amina. Nime . . .

¹⁶ Paulo alisema, “Nikiyaacha mambo hayo nyuma, nakaza mwendo niifikilie mede ya wito mkuu.” Amina. Walipokuwa

wakijiandaa kukikata kichwa chake, na kukatwa kichwa huko Rumi, yeye alisema, “Nimevipiga vita vilivyo vizuri, mwendo nimeumaliza, Imani nimeilinda: Baada ya hayo nimewekewa ta—taji ya haki, Bwana, Hakimu mwenye haki, atanipa wakati wa kuonekana Kwake: si mimi tu, bali wale wote wanaopenda kuonekana Kwake.”

¹⁷ Mnapenda kumwona akija leo? Je, mngpenda kumwona? Na tutakapokutana Naye katika amani, wazieni tu, tutakuwa tumesimama kule, maskini miili hii michafu. Jalia . . . wanaweza kuwa wachanga na wenye ujana, lakini watazeeka. Mvi na ninii . . . na meno yameng’oka, na macho yanafifia, mabega yameinama. Lakini ng’ambo tu ya pazia hili hapa, huyo hapo amesimama mtu mpya kabisa. Maskani hii iliyo ya dunia ikiharibiwa, tunaingia moja kwa moja kwenye ile mpya, namna *hiyo*. [Ndugu Branham anadata vidole vyake—Mh.] Hakika. Kwa kuwa, Yeye yu hai; tunaishi, pia. Nasi tunaishi katika tumaini hili lililobarikiwa.

¹⁸ Kama angeweza kuchukua nyuso zetu asubuhi ya leo, na kuvuta pazia nyuma na kutuonyesha, isingekuwa ni imani tena, basi. Tunaamini tu sasa. Nasi tunahisi, kutoka kwenye Ulimwengu huo mwingine, miangwi ya Utukufu ikirudi nafisini mwetu, ikionyesha, “Ni kweli! Ni kweli! Kaza mwendo uifikilie mede ya wito mkuu!” Ni wakati mzuri jinsi gani! Amina. Loo, Yeye ni halisi sana!

¹⁹ Sasa, jamani, wakati wa kufunga ibada umekaribia sana. Nasi tunawatakeni mpate kiamshakinywa chenu, mrudi upesi sasa kwa—kwa ajili ya kuendeleza ibada. Nimegusia mipaka yake leo, nitaninii . . . na kufikia ufufuo. Lakini asubuhi ya leo, katika saa chache hivi; nataka kwenda nyumbani na kujifungia kabisa kwa ajili ya maombi sasa, kwa kuwa na—naomba ya kwamba Mungu atatupa mstari halisi sana, sana wa maombi leo. Na—na halafu ninataka kuhubiri, baada ya kitambo kidogo, yapata saa kadhaa kuanzia sasa, juu ya kupaa, yale aliyofanya alipopaa juu. Tunaona kile alichofanya hapa kwa gharama, sasa tunataka kuona kile alichofanya alipopaa juu, na yale Mungu aliyofanya kupitia Yeye, na kile alichio leo.

²⁰ Bwana na awabariki, ndilo ombi langu. Kila mtu anauhisi ufufuo? Je, unahisi tu ufufuo moyoni mwako?

²¹ Vema. Na tuinamishe vichwa vyetu kwa ajili ya maombi. Ndugu Neville, sijui kama ungeturuhusu tufumukane, kwa maombi, tafadhali, huku tumeinamisha vichwa vyetu. Mungu akubariki, ndugu. 

56-0401s Mapambazuko Ya Pasaka
Branham Tabernacle
Jeffersonville, Indiana Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org